JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

Simu: +255262963470
Nukushi: +255262963117
Barua pepe: **ps@mit.go.tz**
Tovuti: **www.mit.go.tz**

Mji wa Serikali,
Mtumba,
Mtaa wa Viwanda,
S. L. P 2996,
**40478 DODOMA**.

## TAARIFA KWA UMMA

## MWENENDO WA BEI ZA BIDHAA MUHIMU NCHINI KWA KIPINDI CHA MWEZI SEPTEMBA 2023

**UTANGULIZI**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Kama tunavyofahamu Wizara ya Viwanda na Biashara inatekeleza jukumu la kufanya tathmini na kuratibu ukusanyaji wa takwimu za mwenendo wa bei za mazao ya chakula na bidhaa muhimu nchini. Kutokana na umuhimu wa taarifa hizi kutumiwa na watoa maamuzi, wazalishaji, wawekezaji, wafanyabiashara na wananchi kwa ujumla, Wizara inaendelea kuutaarifu Umma kuhusu tathmini ya bei hizo. Vilevile, Serikali inaendelea kuchukua hatua mbalimbali na stahiki katika kudhibiti ongezeko la bei za bidhaa muhimu nchini. Hatua hizo ni pamoja na kuongeza kasi ya upatikanaji wa bidhaa husika sokoni, kukaa na wazalishaji wa bidhaa mbalimbali hasa za viwandani na kushughulikia kwa haraka changamoto wanazokumbana nazo zinazopelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa husika; Wizara kupitia Tume ya Ushindani pia inafuatilia kwa karibu mienendo ya wazalishaji na wasambazaji wa bidhaa sokoni ili kuzuia mbinu hadaifu zinazoweza kupelekea kupanda kwa bei za bidhaa sokoni.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Baada ya maneno haya ya utangulizi, napenda sasa kuwaletea uchambuzi wa mwenendo wa bei za bidhaa muhimu kwa kipindi cha mwezi Septemba, 2023 kama ifuatavyo: -

## 1. MWENENDO WA BEI ZA MAZAO NA BIDHAA ZA VYAKULA

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Katika taarifa hii ya mwenendo wa bei za mazao na bidhaa za vyakula, tutaangalia mazao ya mahindi, mchele, maharage, na viazi mviringo. Bidhaa nyingine za vyakula tutakazochambua ni unga wa mahindi, unga wa ngano, mafuta ya kupikia pamoja na sukari.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

### i. Mahindi

Bei ya mahindi kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya Shilingi 750 na 1,500 kwa kilo. Bei ya juu ya mahindi imeonesha uhimilivu ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Agosti 2023 ambayo pia ilikuwa Shilingi 1,500 kwa kilo. Hata hivyo, bei ya chini ya mahindi imepungua kwa asilimia 11.8 sawa na kupungua kwa Shilingi 100 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya chini ya mahindi ya mwezi Agosti ambayo ilikuwa Shilingi 850 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Iringa na bei ya juu imeonekana katika Mikoa ya Mara na Kilimanjaro. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya mahindi nchini umepungua kwa asilimia 1.7 kwa mwezi Septemba 2023 ukilinganisha na wastani wa bei ya mahindi kwa mwezi Agosti 2023.

### ii. Unga wa Mahindi

Bei ya Unga wa mahindi kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya Shilingi 1,350 na 2,033 kwa kilo. Bei ya juu ya unga wa mahindi imepungua kwa asilimia 1.6 ambayo ni sawa na kupungua kwa shilingi 34 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya juu ya unga wa mahindi ya mwezi Agosti, 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 2,067 kwa kilo. Hata hivyo, bei ya chini ya unga wa mahindi kwa mwezi Septemba, 2023 imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika ukilinganisha na bei ya chini ya unga wa mahindi kwa mwezi Agosti, 2023. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Manyara na bei ya juu ipo katika mkoa wa Mara. Wastani wa bei ya unga wa mahindi nchini umeshuka kwa asilimia 2.4 kwa mwezi Septemba 2023 ukilinganisha na wastani wa bei ya unga wa mahindi kwa mwezi Agosti 2023.

**iii. Mchele**

Bei ya mchele kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya shilingi 1,900 na 3,500 kwa kilo. Bei ya juu ya mchele kwa mwezi Septemba 2023 imepanda kwa asilimia 2.9 sawa na ongezeko la Shilingi 100 kwa kilo ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 3,400 kwa kilo. Vilevile, Bei ya chini ya mchele kwa mwezi Septemba 2023 imeongezeka kwa asilimia 4.1 sawa na kuongezeka kwa Shilingi 75 ikilinganishwa na bei ya chini ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 1,825 kwa kilo. Mkoa wenye bei ya chini ya mchele ni Katavi wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Arusha. Ukiangalia wastani wa bei ya mchele nchini, uchambuzi unaonesha kuwa wastani wa bei ya mchele kwa mwezi Septemba 2023 umepanda kwa asilimia 3.0 ukilinganisha na wastani wa bei ya mchele kwa mwezi Agosti 2023.

**iv. Maharage**

Bei ya maharage kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya shilingi 2,000 na 3,400 kwa kilo. Bei ya juu ya maharage imepungua kwa asilimia 2.9 sawa na kupungua kwa shilingi 100 ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 3,500 kwa kilo. Bei ya chini ya maharage imeonesha uhimilivu kwa kutobadilika ukilinganisha na bei ya chini ya maharage ya mwezi Agosti

2023. Bei ya chini inapatikana katika mkoa wa Kagera wakati bei ya juu ipo katika mkoa wa Pwani. Uchambuzi wa wastani wa bei ya maharage nchini unaonesha kuwa wastani wa bei ya maharage kwa mwezi Septemba 2023 imepanda kwa asilimia 3.1 ukilinganisha na wastani wa bei kwa mwezi Agosti 2023.

### v. Viazi Mviringo

Bei ya Viazi Mviringo kwa mwezi Septemba ni kati ya shilingi 750 na 1,500 kwa kilo. Bei ya juu ya viazi mviringo kwa mwezi Septemba 2023 imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 1,500 kwa kilo. Hata hivyo, bei ya chini ya viazi mviringo kwa mwezi Septemba 2023 imeshuka kwa asilimia 6.3 ambayo ni sawa na kushuka kwa Shilingi 50 kwa kilo ukilinganisha na bei ya chini ya mwezi Agosti 2023 iliyokuwa Shilingi 800 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Iringa, wakati bei ya juu ipo katika Mikoa ya Manyara na Dar es Salaam. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya viazi mviringo nchini kwa mwezi Septemba 2023 imeshuka kwa asilimia 0.5 ukilinganisha na wastani wa bei ya viazi mviringo kwa mwezi Agosti 2023.

### vi. Unga wa Ngano

Bei ya unga wa ngano kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya shilingi 1,700 na 2,000 kwa kilo. Bei ya juu ya unga wa ngano kwa mwezi Septemba 2023 imepungua kwa asilimia 14.9 sawa na kupungua kwa Shilingi 350 kwa kilo ukilinganisha na bei ya juu ya mwezi Agosti 2023 ambayo ni Shilingi 2,350 kwa kilo. Vilevile, bei ya chini ya unga wa ngano imepungua kwa asilimia 10.5 sawa na kupungua kwa Shilingi 200 kwa kilo ukilinganisha na bei ya chini ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 1,900 kwa kilo. Bei ya chini ipo katika mkoa wa Manyara, wakati bei ya juu ipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Katavi, Kilimanjaro, Pwani, Ruvuma na Singida. Wastani wa bei ya unga wa ngano

nchini kwa mwezi Septemba 2023 umeshuka kwa asilimia 0.5 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo nchini kwa mwezi Agosti 2023.

### vii. Sukari

Bei ya sukari kwa mwezi Septemba ni kati ya shilingi 2,800 na 3,200 kwa kilo. Bei ya juu na ya chini ya sukari kwa mwezi Septemba zmeonesha uhimilivu kwa kutokubadilka ikilinganishwa na bei hizo kwa mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa Shilingi 2,800 na 3,200 kwa kilo mtawalia. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Manyara, wakati bei ya juu ipo katika Mkoa wa Dodoma. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya sukari nchini kwa mwezi Septemba 2023 ni himilivu na haijaonesha mabadiliko yoyote ukilinganisha na wastani wa bei ya sukari nchini kwa mwezi Agosti 2023.

### viii. Mafuta ya Kupikia

Bei ya mafuta ya kupikia ya Alizeti kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya Shilingi 4,000 na 8,000 kwa lita. Bei ya juu ya mafuta ya kupikia ya Alizeti imeongezeka kwa asilimia 6.7 sawa na ongezeko la Shilingi 500 kwa lita ukilinganisha na bei ya juu ya mafuta ya kupikia ya alizeti ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 7,500 kwa lita. Hata hivyo, bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya alizeti kwa mwezi Septemba 2023 imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika ukilinganisha na bei ya chini ya mafuta hayo kwa mwezi Agosti, 2023. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya alizeti inapatikana katika Mikoa ya Singida, Mwanza na Iringa, wakati bei ya juu inapatikana katika Mkoa wa Dar es Salaam. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya mafuta ya kupikia ya alizeti nchini kwa mwezi Septemba 2023 imepanda kwa asilimia 0.8 ukilinganisha na wastani wa bei ya mafuta hayo kwa mwezi Agosti 2023.

Aidha, bei ya mafuta ya kupikia ya mawese kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya Shilingi 4,000 na 7,000 kwa lita. Bei ya juu ya mafuta ya kupikia ya mawese imepungua kwa asilimia 6.7 sawa na kupungua kwa shilingi 500 kwa lita

kulinganisha na bei ya juu ya mafuta ya mawese kwa mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa kati ya Shilingi 7,500 kwa lita. Hata hivyo, bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya mawese kwa mwezi Septemba 2023 imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika ukilinganisha na bei ya mafuta ya mawese ya mwezi Agosti 2023. Bei ya chini ya mafuta ya kupikia ya mawese inapatikana katika Mkoa wa Iringa, wakati bei ya juu ya mafuta hayo inapatikana katika mkoa wa Lindi.

## 2. MWENENDO WA BEI ZA VIFAA VYA UJENZI

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

### i. Saruji

Bei ya saruji (aina ya 32.5) kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya shilingi 14,833 na 23,125 kwa mfuko wa kilo 50. Bei ya juu ya saruji ya aina hiyo imeongezeka kwa asilimia 0.5 sawa na ongezeko la Shilingi 125 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya juu ya saruji aina hiyo kwa mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 23,000 kwa mfuko wa kilo 50. Vilevile, bei ya chini ya saruji ya aina ya 32.5 imepanda kwa asilimia 9.9 sawa na ongezeko la Shilingi 1,333 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya chini ya mwezi Agosti 2023 iliyokuwa Shilingi 13,500 kwa mfuko wa kilo 50. Mkoa wenye bei ya chini ya saruji aina ya 32.5 ni Lindi, wakati bei ya juu ipo katika Mkoa wa Kagera. Aidha, uchambuzi wa wastani wa bei ya saruji (aina ya 32.5) nchini unaonesha kuwa bei ya saruji aina ya 32.5 kwa mwezi Septemba 2023 umeshuka kwa asilimia 2.4 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo kwa mwezi Agosti 2023.

Kwa upande wa saruji (aina ya 42.5), uchambuzi unaonesha kuwa kwa mwezi Septemba 2023 bei ilikuwa kati ya shilingi 15,667 na 24,500 kwa mfuko wa kilo 50. Bei ya juu ya saruji ya aina hiyo imeongezeka kwa asilimia 2.1 sawa na ongezeko la Shilingi 500 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya juu ya saruji aina hiyo kwa mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 24,000 kwa

mfuko wa kilo 50. Vilevile, bei ya chini ya saruji ya aina ya 42.5 imepanda kwa asilimia 6.9 sawa na ongezeko la Shilingi 1,067 kwa mfuko wa kilo 50 ikilinganishwa na bei ya juu ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikua Shilingi 14,650. Mkoa wenye bei ya chini ya saruji aina ya 42.5 ni Mtwara, wakati bei ya juu ipo katika Mkoa wa Kagera. Aidha, uchambuzi wa wastani wa bei ya saruji (aina ya 42.5) nchini unaonesha kuwa wastani wa bei ya saruji aina ya 42.5 kwa mwezi Septemba 2023 umeshuka kwa asilimia 2.6 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo kwa mwezi Agosti 2023.

**ii. Nondo**

Bei ya nondo mm 10 kwa mwezi Septemba ni kati ya Shilingi 17,000 na 22,250 kwa nondo. Bei ya juu ya nondo mm 10 kwa mwezi Septemba imeongezeka kwa asilimia 1.1 sawa na ongezeko la shilingi 250 kulinganisha na bei ya juu ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 22,000. Bei ya chini ya nondo hizo imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika kulinganisha na bei ya mwezi Agosti 2023. Bei za chini ipo katika Mkoa wa Dodoma, wakati bei ya juu ipo katika Mkoa wa Ruvuma. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya nondo mm 10 kwa mwezi Septemba imepanda kwa asilimia 4.1 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo kwa mwezi Agosti 2023.

Bei ya nondo mm 12 kwa mwezi Septemba ni kati ya shilingi 22,000 na 28,000. Bei ya juu ya nondo mm 12 imepanda kwa asilimia 3.7 sawa na ongezeko la shilingi 1,000 kulinganisha na bei ya nondo hizo kwa mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 27,000 kwa nondo. Vilevile, bei ya chini ya nondo mm 12 kwa mwezi Septemba 2023 imepanda kwa asilimia 4.8 sawa na ongezeko la shilingi 1,000 kulinganisha na bei ya mwezi Agosti 2023 iliyokuwa Shilingi 21,000 kwa nondo. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Dar es Salaam, na bei ya juu ipo katika Mkoa wa Katavi. Uchambuzi wa wastani wa bei ya nondo mm 12 nchini unaonesha kuwa bei yake imepanda kwa asilimia 0.9 ukilinganisha na wastani wa bei ya bidhaa hiyo kwa mwezi Agosti 2023.

### iii. Bati

Bei ya bati nyeupe geji 30 kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya shilingi 21,500 na 30,000. Bei ya chini ya bati nyeupe geji 30 kwa mwezi Septemba 2023 imeongezeka kwa asilimia 2.3 sawa na ongezeko la shilingi 500 kulinganisha na bei ya mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 21,000. Pia, bei ya juu ya bati hizi imepanda kwa asilimia 7.1 sawa na ongezeko la shilingi 2,000 kulinganisha na bei ya mwezi Agosti 2023 iliyokuwa Shilingi 28,000. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Dodoma, wakati bei ya juu ipo katika Mkoa wa Kilimanjaro. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya bati nyeupe geji 30 nchini umeongezeka kwa asilimia 2.9 ukilinganisha na wastani wa bei wa bati hizo kwa mwezi Agosti 2023.

Kwa upande mwingine, bei ya bati nyeupe geji 28 kwa mwezi Septemba 2023 ni kati ya shilingi 31,875 na 38,500. Bei ya chini ya bati nyeupe geji 28 kwa mwezi Septemba 2023 imeongezeka kwa asilimia 6.3 sawa na ongezeko la shilingi 1,875 kwa bati kulinganisha na bei ya chini kwa mwezi Agosti 2023 ambayo ilikuwa ni Shilingi 30,000. Hata hivyo, bei ya juu ya bati hizi imeonesha uhimilivu kwa kutokubadilika kulinganisha na bei ya mwezi Agosti 2023. Bei ya chini ipo katika Mkoa wa Mara, wakati bei ya juu ipo katika Mkoa wa Kilimanjaro. Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa wastani wa bei ya bati nyeupe geji 28 nchini umeongezeka kwa asilimia 1.2 ukilinganisha na wastani wa bei wa bati hizo kwa mwezi Agosti 2023.

## 3. MWENENDO WA MAUZO YA MAZAO KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA KWA MWAKA 2023/2024

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Serikali imekuwa ikihimiza matumizi ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kwenye mazao na bidhaa mbalimbali zinazozalishwa na waweka mali (wakulima) na

kuuzwa kwa kutumika mfumo huu rasmi wa biashara kwa lengo la kuleta tija kwa mauzo ya mazao na bidhaa kwa kuongeza ushindani ili kukuza kipato cha mkulima.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Katika kutekeleza azma hii ya Serikali, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) kwa kushirikiana na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX) imekuwa ikiendesha minada ya mazao mbalimbali yanayohifadhiwa katika maghala yaliyoidhinishwa na WRRB.

Sasa naomba tuangazie kidogo kuhusu takwimu za biashara ya mazao ya mbaazi na kakao iliyofanyika kwa msimu wa mwaka 2023/2024, yaani kuanzia mwezi Julai 2023 hadi sasa, kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Ushirika kama ifuatavyo: -

**i. Mauzo ya Mbaazi**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai 2023 hadi sasa jumla ya kilo 34,102,171 za mbaazi zimeuzwa kwa njia ya minada kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Ushirika katika mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma na Manyara. Katika kipindi hicho, jumla ya minada 19 imefanyika na kiasi cha Shilingi 68,855,875,233.00 za mauzo zilipatikana. Aidha, bei ya kilo moja ya mbaazi katika minada hiyo ilikuwa ni kati ya Shilingi 1,942 na 2,130 ikiwa ni tofauti ya Shilingi 1,000 au chini ya hapo nje ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

**ii. Mauzo ya Kakao**

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Kwa upande wa zao la kakao, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2023 hadi sasa, jumla ya kilo 2,470,090 za kakao ziliuzwa kwa njia ya minada kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala na Ushirika mkoani Mbeya. Katika kipindi hicho jumla ya minada 9 ya kakao ilifanyika na kiasi cha Shilingi 19,060,631,870.00 za mauzo zilipatikana. Aidha, bei ya kilo moja ya kakao katika minada hiyo ilikuwa ni kati ya Shilingi 7,720 na 7,841 tofauti na bei ya kakao ya Shilingi 2,000 kwa kilo inayopatikana nje ya Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

## 4. FURSA ZA MASOKO KWA BIDHAA NJE YA TANZANIA

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Ninapenda pia kuchukua fursa, kuwajulisha Wafanyabiashara na Wananchi kwa ujumla kuwa, Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, imeendelea kufungua nchi na kutafuta fursa nafuu za biashara kwa bidhaa zetu kupitia nyanja mbalimbali ambazo ni pamoja na fursa zilizopatikana kupitia mikataba ya biashara baina ya Nchi na Nchi (bilateral), Kikanda na Kimataifa. Fursa hizo ni pamoja na fursa za kuuza bidhaa na huduma katika masoko ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC); Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) na Eneo Huru la Biashara la Afrika (AfCFTA). Tunazo pia fursa za kuuza katika Nchi mbalimbali rafiki ambazo tumeingia nazo makubaliano ya kibiashara kama vile India, Japan, Marekani (AGOA) na China ambayo imetufungulia soko lake la bidhaa kwa asilimia 98.

Kwa upande wa soko la AfCFTA hadi sasa tumefanikiwa kuhamasisha na kuwajengea uwezo Wafanyabiashara wetu ili waweze kutumia fursa zilizopatikana baada ya Nchi yetu kusaini na kuridhia Mkataba wa Soko la Eneo Huru la Biashara Afrika. Juhudi hizi zimezaa matunda na hadi sasa tayari tuna jumla ya Makampuni Manne (4) ambayo yamepeleka bidhaa

kwenye soko la Algeria (Kahawa), Nigeria (Katani), Morocco (Viungo) na Ghana (Katani).

**Orodha ya Makampuni yanayofanya biashara chini ya Mkataba wa AfCFTA**

| NA. | JINA LA KAMPUNI | BIDHAA | UZITO | NCHI ILIKOKWENDA | TAREHE | HALI HALISI |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Export Trading Company Limited (Etg). | Kahawa | 78,080 Kg | Algeria | 09 Mei, 2023 | Imefika Kupitia Bandari ya Baraki. |
| 2. | Export Trading Company Limited (Etg). | Kahawa | 97,600 Kg | Algeria | 09 Mei, 2023 | Imefika Kupitia Bandari ya Baraki. |
| 3. | Tanzglobal Investment Company Limited | Katani (Sisal Fibre) | 26,000 Kg | Nigeria | 18 Mei, 2023 | Imefika Olive Estate Amuwo Lagos. |
| 4. | Export Trading Company Limited (Etg) | Kahawa | 97,600 Kg | Algeria | 20 Juni, 2023 | Imefika Kupitia Bandari ya Baraki. |
| 5. | Anisia Group | Viungo (Cloves) | | Morocco | 13 Julai, 2023 | Imeshafika |

Hivyo, ninaomba kuchukua fursa hii kuwahimiza Wafanyabiashara wetu kujipanga vizuri na kuchangamkia fursa hizi ipasavyo kwa kuzalisha kwa wingi bidhaa zenye ubora na viwango vinavyohitajika sokoni ili tuendelee kunufaika na juhudi anazozifanya Mheshimiwa Rais za kutafuta fursa hizo. Kwa sasa bado hatujafanikiwa kutumia fursa hizo kikamilifu ingawa juhudi mbalimbali zinaendelea kuchukuliwa za kuboresha uzalishaji viwandani na Sekta ya Kilimo zimeonyesha kuzaa matunda ingawa bado sio kwa kiwango tarajiwa.

Kwa mfano, kwenye Soko la EAC katika mwaka 2022, tuliuza bidhaa zenye thamani ya Dola za Marekani Milioni 1,414.9 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 1,161.2 mwaka 2021 ikiwa sawa na ongezeko la a silimia 17.93. Soko la SADC kwa mwaka huo wa 2022 tuliuza bidhaa zenye dhamani ya Dola za Marekani Milioni 1,802.2 ikilinganishwa na Dola za Marekani Milioni 1,303.4 mwaka 2021 ambayo ni sawa na ongezeko asilimia 38.2. Thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda nchi za Bara la Asia hususani kwa nchi za China, India, Japan na Umoja wa Falme za Kiarabu iliongezeka kwa asilimia 64.4 hadi kufikia Dola za Marekani Milioni 4,276.4 kutoka Dola za Marekani milioni 2,601.5 mwaka 2021. Mwaka 2022, mauzo ya bidhaa za Tanzania kwenda Marekani kupitia Mpango wa AGOA yalikuwa jumla ya dola za Marekani milioni 49.05 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 33.04 kwa mwaka 2021 sawa na ongezeko la asilimia 49.8. Serikali imeweka miundombinu wezeshi ya kuyafikia masoko haya, na sasa mpira upo kwa Sekta Binafsi kuona ni jinsi gani wanatumia fursa hizi za masoko ndani ya Bara la Afrika na hata nje ya mipaka ya Bara letu la Afrika.

## 5. HITIMISHO

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Katika kuhitimisha taarifa hii, napenda kutoa msisitizo katika maeneo mawili; **Mosi;** Ni kuhusu soko zuri lililopo kwa bidhaa za mazao, niwaombe watanzania wenzangu tuhakikishe tunauza ziada na tubakishe chakula kitakachotosheleza mahitaji hadi msimu ujao kwani tukiuza chakula chote tunaweza kuja kukinunua kwa bei kubwa zaidi kuliko bei tunayouzia hivi sasa. Aidha, niwaombe Wafanyabiashara wetu wa nafaka tununue nafaka kwa wingi katika maeneo yenye nafaka za ziada na kuzisambaza kwenye maeneo ambayo yanaupungufu wa nafaka hizo, hatua hii itasaidia wananchi kupata fursa ya kununua chakula mapema na kwa bei nafuu ukilinganisha na miezi ijayo ya msimu wa kilimo.

**Pili,** ni kuhusu kuenea kwa Makampuni ya Wakala ambao wanatoa matangazo ya kuandaa safari za kibiashara nje ya nchi na kuwalaghai wafanyabiashara na Wananchi kutoa kiasi cha fedha kama sehemu ya gharama za kujisajili ili waweze kushiriki katika ziara hizo. Matapeli hao wanawaelekeza wafanyabiashara kutuma fedha hizo kwenye simu zao binafsi na akaunti zao binafsi kwenye Mabenki. Hivyo, niwakumbushe watanzania wenzangu kuwa makini na matapeli hawa. Serikali imeshabaini na itawachukulia hatua kali za kisheria wale wote watakaokamatwa kwenye mchezo huu. Pia niwaombe Wafanyabiashara na wenye viwanda nchini tunapoyaona matangazo haya kabla ya kufanya chochote ni vema ukajiridhisha kwa kupata taarifa za fursa hizi kutoka kwenye Mamlaka za Serikali ikiwemo Taasisi yetu ya Maendeleo ya Biashara (Tantrade) ambao ndiyo Taasisi yenye Mamlaka kisheria ya kuratibu masuala yote yanayohusu Maonesho na misafara ya kibiashara iwe ndani au nje ya Nchi yetu.

**Ndugu Waandishi wa Habari;**

Napenda kuendelea kutoa rai kwa wazalishaji wa bidhaa zote za viwandani kuendelea kuongeza jitihada za uzalishaji wa bidhaa wanazozizalisha kwa kuzingatia ubora unaohitajika sokoni na kwa kufuata Sheria, Kanuni na Taratibu zilizowekwa ili kukabiliana na kupanda kwa bei za bidhaa mbalimbali nchini. Pia,

ninawashauri wakulima na wazalishaji nchini, kuuamini na kuutumia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala ili waweze kupata manufaa na kuongeza tija ya mauzo ya mazao na bidhaa zao.

**…………………………………………**

**Dkt. Ashatu K. Kijaji (Mb)**

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA**

**SEPTEMBA, 2023**